

**TUNDURU AGRICULTURAL MARKETING CO-OPERATIVE UNION
(TAMCU LTD REG. NO. 5490)**

TELEPHONE NO. 025-2680850
Email: tamcutunduru@gmail.co

P.O.BOX 299
Tunduru –
Ruvuma



**TAARIFA YA HITIMISHO KWA MINADA YA UFUTA MSIMU WA MWAKA
2023/2024**

1. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015 pamoja na Masharti ya TAMCU Ltd baadhi ya madhumuni ya Chama Kikuu ni pamoja na:

- a) Kununua, kuuza na kusambaza pembejeo za kilimo kwa wanachama wake kwa bei nafuu;
- b) Kukusanya na kuuza mazao kwa lengo la kuyauza kwa faida ya wanachama wake;
- c) Kuanzisha na kuendeleza mitandao mizuri na imara ya kilimo bora cha mazao ya kilimo;
- d) Kutoa elimu ya Ushirika kwa wanachama wake na kuwaendeleza Watendaji wa Chama ili kuleta ufanisi mzuri na kuimarisha uchumi wa chama; na
- e) Kufanya mambo mengine yaliyo halali na ambayo ni ya lazima katika kuendeleza kazi zilizotajwa hapo juu katika kufanikisha utekelezaji wa dhumuni la Chama kama yatakavyopitishwa na Mkutano Mkuu.

2. MAKISIO YA UKUSANYAJI WA UFUTA MSIMU WA 2023/2024

Chama Kikuu kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa msimu wa mwaka 2023/2024 kiliweka malengo ya kukusanya ufuta ufuta kilo **3,822,561**.

Aidha, Chama Kikuu kinapenda kutoa taarifa kuwa Chama kimevuka malengo ya Ukusanyaji kwa Zaidi ya asilimia **20.38%** ya Lengo ambapo kwa msimu huu (*Kuanzia mnada wa I hadi VI*) kimekusanya kilo **4,800,997.20**

3. TAARIFA YA MAKUSANYO YA UFUTA MSIMU WA 2023/2024

Msimu wa Mauzo ya Ufuta wilayani ya Tunduru ulianza rasmi tarehe 15.05.2023 kwa kuanza na zoezi la ukusanyaji wa ufuta katika ghala za Vyama vya Ushirika vya Msingi. Ambapo, mnada wa kwanza wa ufunguzi ulifanyika tarehe 01.06.2023 katika Kijiji cha Lukumbule, Kata ya Lukumbule Wilayani Tunduru.

Katika mnada huo jumla ya kilo za Ufuta **857,977.7** ziliuzwa kwa bei wastani ya shilingi **3,822/-** ukilinganisha na msimu uliopita wa mwaka 2022/2023 katika mnada wa kwanza ufuta kilo **1,008,638** ziliuzwa Kwa bei wastani ya shilingi **2,982/-**.

Aidha, Uzalishaji umeongezeka kutoka kilo **2,548,815** zilizozalishwa msimu wa 2022/2023 hadi kilo **4,800,997.20** zilizozalishwa msimu wa 2023/2024 kutoka mnada wa kwanza hadi mnada wa sita (06) ambapo ni sawa na ongezeko la Asilimia **46%.91** la uzalishaji.

Vilevile, bei imeendelea kuimarika kutoka bei wastani ya shilingi **3,019.80/-** kwa msimu wa 2022/2023 hadi shilingi **3,618.98/-** kwa msimu wa 2023/2024 kuanzia mnada wa kwanza hadi sita (06) ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia **16.56%**

Jedwali kuonesha Mwenendo wa minada msimu wa 2022/2023 na 2023/2024

NAMBA YA MNADA	KGS		BEI WASTANI	
	2022/2023	2023/2024	2022/2023	2023/2024
1	1,008,638	857,977.70	2,982	3,822.00
2	507,522	786,329.00	3,022	3,895.00
3	670,040	1,060,234.50	3,095	3,808.34
4	220,302	925,354.00	3,100	3,497.00
5	142,313	770,760.00	2,900	3,475.00
6	-	240,818.50	-	3,473.00
7	-	159,523.50	-	3,500.00
	2,548,815	4,800,997.20		

NB* Bei wastani 3,019 wastani kwa Msimu 2022/2023 na 3,638 kwa msimu wa 2023/2024

4. MCHANGO WA TOZO MBALIMBALI KUTOKANA NA MAUZO YA UFUTA MSIMU 2023/2024 KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI

Katika msimu wa Ufuta wa mwaka 2023/2024 wadau mbalimbali wameendelea kunufaika kutokana na matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani katika mauzo ya ufuta. Mfano; Wakulima wameendelea kuona uimarikaji wa bei ambao ni muhimu kwa wakulima, Upatikanaji rahisi wa takwimu za mazao yanayozalishwa, Urahisi wa ukusanyaji wa mapato ya serikali na wadau wengine.

Aidha, wadau mbalimbali wameendelea kunufaika kwa kupata tozo stahiki ambazo ni muhimu katika maendeleo kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini; -

NA	TAREHE	MNADA	KILO	AMCOS*TSH 67	UNION*TSH 33	TCDC*5	WRRB*3.3	HALMASHAURI*75
1	01.06.2023	1	857,978	57,484,526	28,313,274	4,289,890	2,831,327	64,348,350
2	08.06.2023	2	786,329	52,684,043	25,948,857	3,931,645	2,594,886	58,974,675
3	15.06.2023	3	1,060,235	71,035,712	34,987,739	5,301,173	3,498,774	79,517,588
4	22.06.2023	4	925,354	61,998,718	30,536,682	4,626,770	3,053,668	69,401,550
5	06.07.2023	5	770,760	51,640,920	25,435,080	3,853,800	2,543,508	57,807,000
6	13.07.2023	6	240,819	16,134,840	7,947,011	1,204,093	794,701	18,061,388
7	JUMLA		4,641,474	310,978,758	153,168,642	23,207,370	15,316,864	348,110,550

4. HITIMISHO

Mwisho, TAMCU inapenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa **Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Wakili. Julius Mtatiro** kwa kutusimamia na kutupatia ushauri wa mara mara ili kuendeleza shughuli za ushirika na tunakuomba uendelee kutusimamia na kutuongoza katika msimu huu wa 2023/2024.

Aidha, TAMCU inapenda kuwashukuru Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Leseni ya Stakabadhi za Ghala, Mabenki, Wasafirishaji, Wanunuzi Pamoja na wadau wengine wote kwa kuendelea kushirikiana na sisi na tunawaomba muendelee kutoa ushirikiano kwa lengo la kusogeza mbele gurudumu la maendeleo.

NAOMBA KUWASILISHA

USHIRIKA PAMOJA TUJENGE UCHUMI

**IMEANDALIWA NA
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA TUNDURU
27, JULAI 2023**